# JOTOARDHI JARIDA

TGDC

## NAIBU WAZIRI MKUU MHESHIMIWA DK.DOTO BITEKO ASEMA-TUMEAMUA KWA DHATI KUENDELEZA MIRADI YA JOTOARDHI

JANU - MACHI 2024

Katika kuhakikisha serikali inatatua changamoto ya upungufu wa nishati ya umeme nchini, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe.Dkt.Doto Biteko amewahakikishia wananchi kuwa, ni muda muafaka kwa serikali kuongeza upatikaji wa nishati ya umeme kupitia vyanzo mbalimbali ikiwemo nishati jadidifu ya jotoardhi.

Dkt. Biteko amesema hayo tarehe 20 Februari, 2024 mara baada ya kukagua vyanzo vya Jotoardhi vya Kiejo-Mbaka (60MW) na Ngozi (MW 70) mkoani Mbeya akifuatana na viongozi mbalimbali wa Mkoa wa Mbeya wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa, Juma Homera.

*"Miradi hii ya Jotoardhi sasa lazima ianze, tutaanza na megawati 10 hapa Kiejo-Mbaka na Ngozi tutaanza na megawati 30 huku nyingine zikifuata"* Alisema Dkt. Biteko.

*"Pamoja na mradi ya jotoardhi, tunakwenda kuzalisha umeme wa jua, upepo, hivyo twende tukajenge vyanzo vingi, tuwe na uwanda mpana wa vyanzo ili tusipate shida, na nimshukuru Mhe.Rais.Dkt.Samia, bwawa la Mwl.Nyerere limekamilika na mashine ya kwanza inatoa umeme, tunakamilisha hatua za kuuingiza kwenye Gridi ya Taifa ili tuanze kuutumia: hivyobasi Watanzania tuvumilie ili tukamilishe"*, aliongeza Mhe.Dkt.Biteko

Mhe. Dkt.Biteko alihitimisha kwa kutoa wito kwa wananchi walio kwenye maeneo yaliyo na rasilimali ya jotoardhi kutoa ushirikiano kwa serikali ili wasicheleweshe utekelezwaji wa mradi akisema kuwa yeye na Mhe.Rais wanakerwa sana na kukatika kwa umeme.

Pia Dkt. Biteko Amewaelekeza watendaji wa Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania (TGDC) kufanya kazi zinazoleta matokeo kwani Serikali inatafuta fedha za kutekeleza miradi hiyo na wajibu wa watendaji wa Taasisi hiyo ni kuhakikisha miradi hiyo inafanikiwa.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Mhe.Juma Homera amesema, kama mkoa wataendelea kumuunga mkono Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kuwa pale anapogundua chanzo chochote cha nishati ya umeme watakilinda kama ilivyo Kiejo-Mbaka na Ngozi lakini pia kuyatunza mazingira ya Mbeya na kwamba hiyo ni mipango ya mkoa huo ili jotoardhi iendelee kutamalaki mpaka hapo ambapo katizo la umeme litakuwa historia nchini, huku akizipongeza



Awali akitoa maelezo mafupi juu ya miradi hiyo, Meneja Mkuu wa Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania TGDC Mha. Mathew Mwangomba amesema, mradi wa Kiejo-Mbaka una lengo la kuzalisha megawati 60 ambapo awamu ya kwanza itaanza na megawati 10 na ya pili kumalizia megawati 50 zitakazobakia na kwamba endapo utakamilika utaongeza usalama wa upatikanaji wa umeme, pia ni rafiki wa mazingira na utatekelezwa kwa kufuata sharia, kanuni na taratibu zote za nchi.

Mha. Mwangomba aliongeza kuwa, uendelezaji wa miradi ya jotoardhi unapitia katika hatua za tafiti za kijiosayansi yaani Jiosayansi ya Kemia, Fizikia na Jiolojia ya eneo husika na kumhakikishia Waziri huyo kuwa vyote hivyo vimefanyika tena kwa kutumia rasilimali watu wa ndani kwa kushirikiana na mashirika ya wahisani. Vilevile, alitumia nafasi hiyo kuishukuru serikali ya Tanzania na mfuko wa maendeleo wa Umoja wa Afrika (GRMF) kwa kuwezesha upatikanaji wa fedha.

Mhandisi Mwangomba alimaliza kwa kusema, TGDC ni lazima itoe umeme.

Ziara hiyo imehudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali mkoa wa Mbeya,-mwenyekiyi wa bodi ya TGDC, machifu, wananchi, watumishi wa wizara ya nishati pamoja na watumishi wa TGDC.





# TANZANIA KUWA MWENYEJI WA KONGAMANO LA KUMI LA KIKANDA LA JOTOARDHI AFRIKA ( ARGeo – C10)



Na Mwandishi wetu

NCHI ya Tanzania inatarajia kuwa mwenyeji wa kongamano la 10 la kikanda la jotoardhi ambapo takribani washiriki 1000 kutoka mataifa mbalimbali wanatarajiwa kushiriki.

Hayo yamebainishwa jijini Dar es salaam leo Machi 18, 2024 na Kamishna wa Umeme na nishati jadilifu kutoka Wizara ya Nishati ,Mhandisi Innocent Luoga wakati akifungua mkutano wa maandalizi ya kongamano hilo.

Amesema kongamano hilo linatarajiwa kufanyika Novemba 11 hadi 17 mwaka 2024 huu ambapo nchi zaidi ya 50 zinatarajiwa kushiriki.

*"Kongamano hili la uendelezaji wa jotoardhi katika nchi za ukanda wa Mashariki ya Afrika ambapo katika nchi hizo zipo nchi sita wanachama katika ukanda ambazo ni pamoja na Tanzania, Kenya, Uganda, Ethiopia, Rwanda, Djibouti"* amesema mhandisi Luoga.



Amesema washiriki wa kongamano hilo ni wataalamu wa jotoardhi pamoja na wafadhili wa miradi, na sekta binafsi za kuendeleza miradi mbalimbali.

*"Nchi ya Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano huu ni baada ya mwaka 2022 Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kukubali ombi la Shirika la kimataifa la mazingira (UNEP) la Tanzania kuwa mwenyeji wa kongamano hilo ambalo hufanyika kila baada ya miaka miwili katika nchi mwanachama"* amesema Mhandisi Luoga

Akitaja faida za kongamano hilo kufanyika hapa nchini Mhandisi Luoga amesema ni pamoja na kuharakisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya jotoardhi inayotekelezwa. Sambamba na kuasaidia kubadilishana uzoefu na utaalamu mbalimbali katika utekelezaji wa miradi mbalimbali

Aidha amesema nchi ya Tanzania ina rasilimali ya jotoardhi ambayo inaweza kuzalisha megawati za umeme zaidi ya 5000. Mhandisi Luoga ameeleza kuwa sera ya nishati inataka uzalishwe umeme kwa kutumia vyanzo mchaganyiko ili kuwa na umeme wa uhakika.

*"Sasa tunataka kuzalisha umeme kwa kutumia jotoardhi tunatambua nchi yetu kwa sasa inazalisha umeme kwa kutumia maji, gesi pamoja jua"* amesema Amesisitiza kuwa Tanzania kuwa mwenyeji wa kongamano hilo ni Moja ya mikakati ya kuhakikisha inakuwa na umeme wa uhakika na salama katika nchi bila ya kuathiri shughuli za kijamii na kiuchumi.

Aidha amesema kongamano hilo pia litaweza kuleta matokeo makubwa ikiwemo kuitangaza TGDC pamoja na kukaribisha wafadhili kwa ajili ya kufanya tafiti.



# TGDC KUCHIMBA VISIMA VYA KUZALISHA UMEME WA JOTOARDHI KATIKA MRADI WA NGOZI MBEYA.

Katika kuhakikisha Nishati ya umeme wa uhakika Nchini, Kampuni ya uendelezaji jotoardhi Tanzania TGDC Imeanza mchakato wa kuchoronga visima vya utafiti ili kuhakiki kiwango cha rasilimali ya Jotoardhi itakayoweza kuzalisha umeme katika eneo la Ziwa Ngozi mkoani Mbeya.

Akizungumza katika mkutano wa siku tatu wakimataifa ulioandaliwa na kampuni hiyo na kuwahusisha wanasayansi wabobezi wa Jiofizikia, Jiokemia na Jiolojia kwa lengo la kuthibitisha taarifa za kisayansi za uwepo wa jotoardhi linaloweza kuzalisha umeme katika eneo la mradi wa Ngozi, Meneja mkuu wa Kampuni ya hiyo Mhandisi Mathew Mwangomba alisema kuwa, sayansi imeonyesha uwepo wa joto ardhi katika eneo la Ngozi, Lengo ikiwa ni kuongeza vyanzo mbadala vya umeme ili kuinua uchumi pamoja na kupambana na Mabadiliko ya tabia nchi kwa kuongeza uhakika wa Umeme uliobora ifikapo 2025.

*"Sayansi zetu zinatuthibitishia kwamba kuna rasilimali ya jotoardhi katika eneo letu la Ngozi na Tunatambua kwamba Umeme ni uchumi, burudani kwa kifupi umeme ni kilakitu kwa maisha ya Sasa"* Aliongeza Mhandisi Mwangomba.

Vilevile, Mhandisi Mwangomba alisema, *"Serikali yetu ina maono ya 2025 ambayo yananazungumzia upatikanaji wa nishati ya umeme ambayo TGDC ndio kiranja wa kuhakikisha umeme unapatikana, Hivyo basi sisi jukumu letu ni kuhakikisha kwamba tuweze kuiletea Nchi yetu Umeme uliobora, imara ili kukuza uchumi wa mtu mmojammoja na Taifa kwa ujumla".*






Tunapokwenda ngozi tunaenda kuhakiki uwepo wa rasilimali ya Jotoardhi tulijiwekea malengo ya kuchimba taratibu zinaendelea lakini wataalamu wetu wapo katika eneo la tukio.

Eneo la ngozi ni muhimu kwasababu ni eneo la Kivolkano hai" Amesema Mathew.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara wa Kampuni hiyo Mha. Shakiru kajugus alisema, hatua ya uchorongaji ni moja kati ya hatua za kupata umeme unaotokana na Jotoardhi ambapo mradi wa Ngozi ulioanza kufanyiwa utafiti tangu mwaka 2015. Hata hivyo, TGDC ilijipangia kuwa, ifikapo 2025 uwe muda muafaka kwa wao kuzalisha umeme wa kwanza wa Jotoardhi ambapo wanatarajia kuzalisha megawati 70 katika hatua mbili tofauti.

*"Tanzania imebarikiwa kupitiwa na bonde la ufa na ina rasilimali kubwa saana ya Jotoardhi.*
*Mradi wa ngozi umeanza kufanyiwa utafiti tangu 2015 na tumejipangia mpaka 2025 tutakuwa na umeme wa kwanza wa jotoardhi"*

Tunatarajia kuzalisha Megawati 70 za umeme ambapo kwa hatua ya kwanza tunaanza na
Megawati 30 na baadae 40, kisha tutaendelea" Alisema Kajugus.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Mkuu wa mkoa katika mkutano huo Mh.Alhaj Mbarack Batenga ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Chunya aliwataka wakazi wa Mbeya na Tanzania

kuchangamkia fursa zitakazojitokeza kwani kuwepo kwa jotoardhi katika eneo hilo ni Fursa kwa mnyororo wa huduma.

*"Nimeona hapa na niwapongeze TGDC kwa kuandaa mkutano huu mkubwa, kwani umeme wa jotoardhi unaenda kukwamua kadhia ya kukatika kwa umeme. Kuwepo kwa chanzo cha umeme wa jotoardhi ni ajira na ni fursa kwa kuwa kuna mnyororo wa huduma, hivyo tutapata manufaa makubwa katika mkoa wetu wa Mbeya. Hivyo ni vyema Tujiandae katika safari hii kwani bado ni ndefu watu tachangamkie hii fursa yenye manufaa kwa nchi yetu".*



# VIONGOZI WA DINI NA MACHIFU WATEMBELEA MIRADI YA JOTOARDHI- MBEYA, WATOA BARAKA

Viongozi wa dini na wawakilishi kutoka madhehebu mbalimbali wakimemo TEC, BAKWATA na CCT pamoja na Machifu mkoani Mbeya, wamefanya ziara katika miradi ya jotoardhi Ngozi na Kiejo-Mbaka, miradi iliyo chini ya Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania TGDC kwa lengo la kujifunza na kupata uelewa juu ya miradi hiyo.

Wakiongea baada ya kutembelea maeneo hayo Machi 12, 2024, viongozi hao walisema wamefurahishwa na walistaajabu kwakuwa pamoja na kuwa mkoani hapo, hawakuwahi kuijua miradi hiyo, hivyo wakaahidi kuendelea kueneza habari kwa waumini wanaowaongoza ili elimu hiyo iwafikie wengi.

Mkuu wa msafara katika ziara hiyo alikuwa Meneja Mkuu msataafu na Kiongozi wa kwanza wa TGDC Mh. Boniphace Njombe alitoa elimu kuhusu TGDC kwa nini ilianzishwa, ilipo na mipango na mategemeo makubwa ya Serikali kuhakikisha rasilimali ya nishati jadidifu ya jotoardhi inapatikana kuiondoa nchi yetu katika changamoto ya upungufu wa umeme.



Kwa upande wake Meneja Mkuu wa Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania TGDC Mhandisi Mathew Mwangomba amebainisha kuwa, ni muhimu sana kwa viongozi wa madhehebu ya dini pamoja na viongozi wa kimila ambao ni machifu kuwa na uwelewa wa pamoja wa upatikanaji wa nishati hiyo ili kusaidia wananchi wengine nao kupata uelewa sawa, na kwamba kwa kufanya hivyo itasaidia jamii kuwa na uelewa wa pamoja juu ya asili na uwepo wa rasilimali hiyo kwenye maeneo yao.









Wakihitimisha ziara hiyo, vongozi hao walimaliza kwa kuomba dua ya pamoja ili utekelezaji wa miradi hiyo ufanyike kwa mafanikio.







## MHE . KAPINGA: TGDC ONESHENI MATOKEO CHANYA KWA KUZALISHA UMEME

Dar Es Salaam

Kampuni ya Uendelezaji wa Joto Ardhi Tanzania (TGDC) imetakiwa kuonesha Matokeo Chanya kwa kuzalisha Umeme kwa kutumia Rasilimali ya Jotoardhi ili kuunga Mkono Mpango wa Serikali wa kuwa na Nishati Safi na Endelevu.

Agizo hilo limetolewa na Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga wakati wa kikao na Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni hiyo pamoja na Menejimenti ikiwa ni sehemu ya muendelezo wa ziara yake ya kikazi ya kukutana na baadhi ya Taasisi na Kampuni zilizo chini ya Wizara ya Nishati kwa lengo la kuona Utendaji kazi wa Taasisi hizo Tarehe 8 Januari 2024, Jijini Dar Es Salaam.

Mhe. Kapinga ameieleza TGDC kuwa wabunifu na kutumia uwezo wao wote kuhakikisha kuwa Kampuni hiyo inaanza kuzalisha umeme kwa kutumia Rasilimali ya Jotordhi kwa kuwa tayari baadhi ya maandalizi yameshafanyika katika maeneo ya vipaumbele.

Amesema kama ambavyo Serikali imejipambanua kuwa inatekeleza Mpango wa Nishati Safi na Endelevu, ni wakati wa TGDC sasa kuonesha uwezo wao katika kufanikisha hilo ili kutoa mchango mkubwa kwa Taifa.

Vilevile amewasisitiza kuwa ili kuhakikisha wanapata matokeo chanya na ya haraka zaidi ni vyema wakaongeza ubunifu, uthubutu, kushirikiana na kutoridhika na kila wanachofanya ili kupiga hatua mbele zaidi. Hali hiyo itaondoa changamoto ya umeme unayoikumba nchi kwa kuzingatia kuwa nishati ya Jotoardhi ni endelevu.





*"Nchi na Watanzania wanataka kuona umeme unaozalishwa kutokana na Jotoardhi,TGDC ni wakati wenu sasa kuonyesha uwezo wenu wa kuleta matokeo Chanya kwa Taifa, tumieni Ubunifu na Uwezo wenu wote kuhakikisha kile mlichokikusudia kinafanikiwa na kuonekana kama Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) inavyoelekeza kuwa uzalishaji wa umeme utaongezeka kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo Jotoardhi, vilevile kuunga mkono Mpango wa serikali wa kuwa Nishati Safi na Endelevu",* alisema Mhe. Kapinga.

Aidha amewapongeza TGDC kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya kuhakikisha umeme unapatikana na pia amewataka kutumia vyema Weledi na Taaluma walio nayo kulinda Kampuni hiyo ili kupata matokeo ya haraka.

*"TGDC lazima muonyeshe mchango wenu Nishati Safi na Endelevu ili Nchi na Dunia ione uwepo wenu na Serikali inataka matokeo hivyo mjikite katika hilo na watanzania wanaamini katika matokeo"* alisisitiza Mhe. Kapinga.

Kwa Upande wake Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Athumani Mbuttuka, amewaeleza TGDC kuwa ofisi yake iko wazi wakati wote ili kupokea changamoto zozote zinazowakabili ili kuwasaidia na kuzitatua pale watakapoona wanakwama katika kutekeleza majukumu yako.

Sambamba na hilo amewataka kushirikiana, kuwa wabunifu na wenye uthubutu kuhakikisha kile walichokikusudia kinafanikiwa na watanzania wanapata umeme.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa TGDC Prof. Shubi Kaijage na Meneja Mkuu wa TGDC, Mha. Mathew Mwangomba wamemuakikishia Naibu Waziri Kapinga kuwa watashirikiana kwa pamoja kuhakikisha wanazalisha umeme wa Jotoardhi haraka iwezekanavyo na wanaendelea kutoa elimu ya Rasilimli ya Jotoardhi kwa wadau mbalimbali ili wawe na uelewa mpana zaidi kuhusu mradi huo wa kimkakati.

Wamesema kuwa kampuni hiyo ina miradi mitano ya kipaumbele ambayo ni ule wa Ziwa Ngozi unaotajiwa kuzalisha Megawati 70 lakini kwa kuanzia wataanza na Megawati 30. Mradi Mingine ni wa Kiejo-Mbaka mkoani Mbeya Megawati 60, Songwe mkoani Songwe Megawati 5 hadi 38, Luhoi mkoani Pwani Megawati 5 na Natroni mkoani Arusha Megawati 60.

Miradi yote hiyo iko katika hatua mbalimbali ambapo nguvu kubwa imeelekezwa katika Mradi wa Ngozi ambapo tayari mtambo wa kuchoronga visima vya Jotoardhi umepelekwa huko na hivi karibuni wataanza kazi ya uchorongaji.

# "TGDC INATAMBUA MCHANGO WA WANAWAKE" ASEMA GOWELE

Kila ifikapo Machi 8 ya kila mwaka, dunia huadhimisha siku ya wanawake duniani, jambo linaloifanya Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania TGDC kushiriki sherehe hiyo kwa kuwakutanisha wanawake wote waajiriwa ndani ya kampuni yake.

Kwa mwaka 2024, TGDC iliwakutanisha watumishi wake wanawake katika jengo la makao makuu ya ofisi yake ambapo wanawake walipata fursa ya kufurahia mafanikio na kubadilishana uzoefu wa kazi.









Akiongea na wanawake hao, Kaimu Meneja Mkuu wa kampuni hiyo ambaye ni meneja rasilimali watu Bi.-Judih Gowele alisema, *"TGDC inatambua mchango wa wanawake na inawekeza kwa wanawake kama kaulimbiu isemavyo na ndiyo maana imetenga siku hii na kuwezesha wanawake wa TGDC kutoka ofisi ya Mbeya na Dar es Salaam kukutana pamoja"*

Bi.Judith aliongeza kuwa, TGDC inaendelea kuboresha maslahi ya wanawake na kwamba ofisi inazingatia suala la usawa wa kijinsia ikiwa ni moja ya nguzo inazozisimamia huku akitoa mfano kwa kampuni hiyo kuwa na mameneja wanawake na wanaochapa kazi vizuri.

Akimalizia hotuba yake, Bi. Judith alisema wanawake wana uwezo mkubwa wa kufanya kazi na kutoa matokeo huku aki inukuu kaulimbiu ya siku ya wanawake duniani ya mwaka 2024 isemayo *"wekeza kwa wanawake: kuharakisha maendeleo ya taifa na ustawi wa jamii"* na kutumia nafasi hiyo kumpongeza Rais wa Tanzania akisema, *"Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, amekuwa ni kiongozi wa mfano, ninyi ni mashahidi kwa namna alivyoipokea nchi na kuendelea hadi hivi sasa, hii inathibitisha kuwa, ANAWEZA na sisi wanawake Tunaweza".*

Maadhimisho ya sherehe za siku hiyo ya wanawake yalihitimishwa kwa wanawake wa TGDC kujumuika na wanawake wengine wa Wizara na Nishati na taasisi zake Jijini Dodoma.



# MATUKIO KATIKA PICHA
# MACHI 2024


















# KAMPUNI YA UENDELEZAJI JOTOARDHI TANZANIA (TGDC) YATEKELEZA CSR KWA VITENDO

Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC), imetoa Elimu, Msaada wa Daftari na Mabegi kwa wanafunzi katika Shule ya Msingi Mbeye 1 kuhusu rasilimali ya Nishati Jadidifu ya Jotoardhi itakayopatikana katika mradi wa Ngozi uliyopo katika Kata ya Isongole, Kijiji cha Mbeye 1, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya.

Mradi huo wa Ngozi, unatarajiwa kuzalisha Megawati 70 za Nishati ya umeme wa Jotoardhi ambapo kwa sasa upo katika maandalizi ya hatua ya uchorongaji wa visima vya jotoardhi

Aidha, TGDC imekabidhi Tenki la Maji ujazo wa Lita 10,000 ili kuondoa adha waliyokuwa wakiipata wanafunzi wa shule hiyo, ambapo hapo awali waliyafuata maji ng'ambo ya barabara, hali iliyokuwa ikihatarisha usalama wao kwani wengine walipata ajali walipokuwa wakivuka upande wa pili.



## MATUKIO KATIKA PICHA

TGDC imefanya tukio hilo ikiwa ni utekelezaji wa takwa la kisheria la uwajibikaji wa kampuni kwa jamii (CSR) kwa kuwa shule hiyo ipo katika kijiji ulipo mradi wa Ngozi na kwa kufanya hivyo, TGDC inaendeleza mahusiano mema baina yake na jamii inayozunguka eneo ulipo mradi














# TGDC YATEKELEZA AHADI YA KATIBU MKUU-NISHATI, MHA. MRAMBA.




Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC) imekabidhi Jezi za mpira na Fulana (T-shirt) kwa kikundi cha ngoma za asili cha Jotoardhi na timu ya mpira wa miguu ya jotoardhi katika kijiji cha Nanyala, Mkoani Songwe tqrehe 22.02.2024, kutokana naahadi ya Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mhandisi Felchesmi Mramba wakati alipo fanya ziara katika mradi huo.

Akiongea kwaniaba ya timu ya mpira na kikundi cha ngoma, bw Imani Juma naDaniel Jakobwalisema, wanaishukuru TGDC kwa kutekeleza ahadi aliyoitoa kiongozi na Katibu Mkuu wa wizara ya Nishati na kwamba, watatumia fursa hiyo kuelimisha jamii juu ya nishati ya Jotoardhi.

TGDC inaendelea kujenga mahusiano mema na jamii inayozunguka miradi inayoisimamia na kwa kufanya hivyo, hadi sasa miradi hiyo inaendelea kutekelezwa kwa uzuri kutokana na jamii kuwa karibu nayo.

Akikabidhi vifaa hivyo kwaniaba ya Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti Pamoja na Watumishi wa TGDC, Afisa Mkuu wa Mawasiliano Bi.Khadija Faru alisema; lengo la kukabidhi vifaa hivyo ni kuteleleza ahadi iliyotolewa na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mhandisi Mramba, aliyoitoa wakati wa ziara yake kukagua maendeleo ya mradi wa rasilimali ya Jotoardhialiyoifanya na kuagiza TGDC iwezeshe vikundi hivyo sare.

*"Ni jambo la kumshkuru Mungu, leo niko hapa kwaniaba ya uongozi wa TGDC kukabidhi jezi na sare mlizoahidiwa na kiongozi wetu ambaye ni Katibu Mkuu wa wizara mhandisi Felchesmi Mramba. Tunaamini mtazitunza na mtazitumia kwa lengo kusudiwa huku mkiisaidia jamii iielewe TGDC ni nini na inafanya nini"*, alisema Bi. Khadija.



